**HOTUBA YA IJUMAA**

**Lugha ya Quran na kulinda asili yake.**

**Imefasiriwa na**

**profesa Ayman Alasar**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitakatifu: **كِتَابٌ فُصِّلَتْ آيَاتُهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِّقَوْمٍ يَعْلَمُونَ**

{**Hichi ni Kitabu kilicho pambanuliwa Aya zake, cha kusomwa kwa Kiarabu kwa watu wanao jua**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki ispokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehema na amani pamoja na baraka kwake pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.

**Baada ya utangulizi**:

Kwa hakika lugha ni uelewa wenye kubeba maana na tamaduni, nayo ni moja ya muhimili wa kujenga asili na kuathiri katika ujenzi wa haiba, mwenye kuzungumza lugha mbili anakuwa amekusanya tamaduni mbili, na mwenye kuzungumza lugha tatu anakuwa pia amekusanya tamaduni tatu, na anasema muundo wa akili nyingi, tofauti na lugha mama ya mwanadamu itaendelea kuwa moja ya muhimili muhimu wa kutengeneza utamaduni wake, mtu ambaye hafahamu siri za lugha yake hawezi kufahamu utamaduni wa watu.

Lugha ya Kiarabu ni maalum sana, kwani ndio lugha ya Quran Tukufu na Sunna Takatifu za Mtume SAW, na imekuwa ni muujiza mkubwa kwa Mtume SAW hii Quran kwa ufafanuzi wake na siri zake za kilugha na kimaelezo, ambapo Anasem Mola Mtukufu:

**إِنَّا أَنزَلْنَاهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لَّعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ.**

{**Hakika tumeiteremsha Quran kwa lugha ya Kiarabu ili mpate kuzingatia**}. Na akasema tena Mola Mtukufu: **وَكَذَٰلِكَ أَنزَلْنَاهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا** {**vile vile tumeiteremsha Quran kwa lugha ya Kiarabu**}. Na akasema Mola Mtukufu: **قُرْآنًا عَرَبِيًّا غَيْرَ ذِي عِوَجٍ لَّعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ** {**Qurani kwa lugha**

**ya Kirabu iliyonyooka ili wapate kumcha Mungu**}. Na anaendelea tena kusema Mola Mtukufu: وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِتُنْذِرَ أُمَّ القُرَى وَمَنْ حَوْلَهَا وَتُنْذِرَ يَوْمَ الجَمْعِ لا رَيْبَ فِيهِ

{**Na namna hivi tumekufunulia Quran kwa Kiarabu ili uwaonye watu wa Mijini na walio pembezoni mwake. Na uwatahadharishe na siku ya mkusanyiko ambayo haina shaka ipo**}. Na Anasema pia Mola Mtukufu; بِلِسَانٍ عَرَبِيٍّ مُبِينٍ {**Kwa lugha ya Kiarabu iliyo wazi**}. Na Anasema tena Mola Mtukufu:

لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ ذِكْرُكُمْ أَفَلا تَعْقِلُونَ.

{**Na hakika tumekuteremshieni Kitabu ambacho ndani yake yamo makumbusho yenu. Je! Hamzingatii?**}.

Quran imeambatanisha kati ya lugha ya Kiarabu na matendo ya akili, akasema Mola Mtukufu: إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ {**Hakika tumeiteremsha Quran kwa lugha ya Kiarabu ili mpate kuzingatia**}. Waislamu wakaenda sambamba na Quran kwani wakaifanya kazi akili zao na wakazalisha ustaarabu usiopingika, kama vile Mwenyezi Mungu ameunganisha kati ya lugha ya Kiarabu na ulinganiaji katika elimu, akasema Mola Mtukufu: كِتَابٌ فُصِّلَتْ آيَاتُهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ {**Hichi ni Kitabu kilicho pambanuliwa Aya zake, cha kusomwa kwa Kiarabu kwa watu wanao jua**}. Kwa maneno haya amehimiza kutafuta elimu akielezea hilo ni kufikia ucha-Mungu, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا القُرْآنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ * قُرْآنًا عَرَبِيًّا غَيْرَ ذِي عِوَجٍ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ.

{**Na bila ya shaka tumewapigia watu mifano ya kila namna katika hii Quran ili wapate kukumbuka * Quran ya Kiarabu isiyo na upogo, ili wamche-Mungu**}.

Hakuna anayepinga kuwa haiwezekani kufahamu dini yetu kwa ufahamu sahihi zaidi wala kufahamu undani wa hukumu zake ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu na Sunna za Mtume wetu Muhammad SAW isipokuwa ni kwa kufahamu lugha ya Kiarabu kwa ufahamu wa kina, kwani lugha ndio funguo ya uelewa katika dini, ambapo anasema Abdillah Ibn Abbas RA: "Nilikuwa sifahamu nini maana ya maeneo ya Mwenyezi Mungu {**Muumba wa mbingu na ardhi**} mpaka waliponijiia watu wawili walikuwa wanagombana eneo la kisimani, mmoja akasema: Mimi ndio nimekianzisha,

isipokuwa watu wa misingi ya dini na wanafiqhi na wengine wameweka uwezekano katika lugha ya Kiarabu na vyombo vyake kuwa ni moja ya masharti ya kufanya jitihada.

Kama vile hakuna anayepinga kwa kutofahamu lugha ya Kiarabu na kutofahamu kwa kina maandiko na kufahamu yanayofungamana na maandiko pamoja na kuishia kufanya kazi ya kuchukuwa mambo juu juu pasi ya kufahamu undani wake na siri zake kunapelekea kwenye kosa kubwa, na hali kupelekea kwa muhusika wake kuwa na ufahamu wenye makosa ambao unapelekea kwenye kuhalalisha umwagani damu, kwa sababu hiyo swala la kufahamu Quran na Sunna ni lazima, ambapo kufahamu huko hakuwi isipokuwa ni kwa kujifunza lugha ya Kiarabu, chenye kupelekea kutimiza wajibu nacho ni wajibu, na Omar Ibn Khattab RA alikuwa anasema: “Jifunzeni lugha ya Kiarabu kwanye yenyewe ni sehemu ya dini yenu, akawaamrisha watu wajifunze kurusha mkuki na wanakosea, wakasema sisi bado tunajifunza, ndipo Omar aliposema, kukosea kwenu katika lugha yenu ndio mbaya zaidi kwangu kuliko kukosea kurusha kwenu, na anasema Abdul-Malik Ibn Marwan RA: Fanyeni vizuri lugha zenu kwani mtu anawakilishwa na muakilishi na kuazima nguo na mnyama, lakini haiwezekani kuazima lugha, na uzuri wa mtu ni ufasihi wake.

**Hotuba ya pili:**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehema na amani zimwendee mbora wa viumbe naye ni Mtume wetu Muhammad pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa lugha ya Quran inakusanya urithi wa umma na kuulinda, na kuibua fikra na tamaduni kwa kipindi chote, na kuifanya fikra ya umma kubakia muda wote, na kuwepo kwa mataifa kunafungamana na uwepo wa lugha yake, kwani umma ambao lugha yake imepotea basi umma huo umeondoka kwenye uwepo, hivyo kuipa umuhimu lugha kunazingatiwa ni kiashirio miongoni mwa viashirio vya kupewa umuhimu asili yake na kulindwa, kwani lugha ndio yenye kueleza umoja na umoja wa lengo pamoja na umoja wa fikra, kama vile lugha ndio ufahamu muhimu wa kitamaduni kwa umma wowote au tamaduni yeyote.

Tunahitaji zaidi muamko na kupambana na kila jaribio la kuondoa asili ya lugha, na kufanya kazi kwa nguvu kubwa ya kuimarisha ustaarabu wetu katika kupambana na

mawimbi makubwa, kupitia kujitosheleza na lugha ya Quran na kuilinda, kwani ndio funguo ya asili na kujifaharisha nayo, na kuhudumia huduma za dini na taifa.

Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba uhifadhi Misri na kila aina ya ubaya pamoja na zengine za ulimwengu wa Kiislamu na Kiarabu